MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA TAREHE 27 - 28/10/2016 ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA, 2016).

A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	Mh. Namkulya S. Namkulya	-Kata ya Mihambwe	-Mwenyekiti
2.	" Makuyeka B. Salum	-Kata ya Chikongola	-M/Mwenyekiti
3.	" Katani A. Katani	-Mbunge- Tandahimba	-Mjumbe
4.	" Issa Nasoro Kalumbe	-Kata ya Mahuta	"
5.	" Ngerezani Bakari Musa	-Kata ya Kitama	"
6.	" Kawasaki Lipangati	-Kata ya Mnyawa	"
7.	" Simba Nasoro Hashimu	-Kata ya Naputa	"
8.	" Chimale S. Abdallah	-Kata ya Lukokoda	"
9.	" Sharafi Dihoni Hamisi	-Kata ya Malopokelo	"
10.	" Mtimbuka K.Ramandani	-Kata ya Nambahu	"
11.	" Mawazo S. Mbombenga	-Kata ya Nanhyanga	"
12.	" Jamali M.Mtima	-Kata ya Namikupa	"
13.	" Ally D. Nantindu	-Kata ya Michenjele	"
14.	" Nembo H. Mchola	-Kata ya Maundo	"
15.	" Ahmadi A. Ndende	-Kata ya Mkoreha	"
16.	" Ashura m. Ngope	-Kata ya Mchichira	"
17.	" Ramadhani S. Ulaya	-Kata ya Milongodi	"
18.	" Mohamedi T. Ussi	-Kata ya Kwanyama	"
19.	" Selemani Y. Chambengela	-Kata ya Litehu	"
20.	" Ismail S. Chipoka	-Kata ya Ngunja	"
21.	" Zainabu H. Mpota	-Kata ya Mkonjowano	"
22.	" Alafa T. Nakatanda	-Kata ya Mkwiti	"
23.	" Ayubu Mohamedi	-Kata ya Lyenje	"
24.	" Rashidi N. Mtima	-Kata ya Chingungwe	"
25.	" Mfaume H. Abdallah	-Kata ya Miuta	"
26.	" Mkwahe M. Milembu	-Kata ya Chaume	"
27.	" Salumu A. Mnyongo	-Kata ya Dinduma	"
28.	" Abdallah H. Ponela	-Kata ya Luagala	"
29.	" Likapa J.Nangololo	-Kata ya Mndumbwe	"
30.	" Hamisi B. Nayowela	-Kata ya Tandahimba	"
31.	" Fakihi M. Mwango	-Kata ya Mdimba	"
32.	" Yusufu B. Nampoto	-Kata ya Mkundi	"
33.	" Asha R. Tebwa	-Viti Maalum	"
34.	" Halima Tamatama	-Viti Maalum	"
35.	" Huduma S. Mnoda	-Viti Maalum	"
36.	" Amina Issa Mpota	-Viti Maalum	"
37.	" Hadija S. Mnihwika	-Viti Maalum	"
38.	" Shamia M. Kaisi	-Viti Maalum	"
39.	" Fidea A. Hittu	-Viti Maalum	"
40.	" Asia A. Likoba	-Viti Maalum	"
41.	" Rehema C. Liute	-Viti Maalum	"

42.	“	Hawa M. Ramandani	-Viti Maalum	“
43.	“	Amina A. Simba	-Viti Maalum	“
44.	Ndg	Said A. Msomoka	- Mkurugenzi Mtendaji (W)	Katibu

B: **WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA**

1.	Ndg.	Ahmada Suleiman	- Afisa Utumishi (W)
2.	“	Machela A.H	-Mweka Hazina (W)
3.	“	Issa Naumanga	-Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
4.	Eng:	Paul Mlia	-Mhandisi wa Ujenzi (W)
5.	Dr.	Antipas Swai	-Kaimu Mganga Mkuu (W)
6.	Ndg:	Massau A.J	-Afisa Maendeleo ya Jamii
7.	“	Mpangala P.N	-Kaimu Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira (W)
8.	“	Samson Kapange	-Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
9.	“	Lazaro Matoke	- Afisa Utumishi
10.	“	Seleman I. Ng’ambi	-Kny: Afisa Elimu Sekondari (W)
11.	“	Yunus A. Mchala	-Kny: Mhandisi wa Maji (W)
12.	“	Kashen J. Mtambo	-Kaimu Afisa Mipango (W)
13.	“	William Kongola	-Mkaguzi wa ndani wa Hesabu
14.	“	Rajabu C. Athman	-Afisa Utamaduni
15.	“	Abdul J. Masudi	-Kaimu Afisa Elimu (W)
16.	“	Zuberi Sarahani	-Mwanasheria
17.	“	Protas Muhanuzi	-Afisa Manunuzi
18.	“	Ismaely Mbilinyi	-Mratibu wa TASAF
19.	“	James C. Chitumbi	-TEO Tandahimba
20.	“	Nassib N. Shaibu	-TEO Mahuta

C: WAALIKWA

1.	Ndg:	Mohamedi Wasinde	- Afisa Serikali za Mitaa- Mtwara
2.	Mh.	Sebastian Waryuba	-Mkuu wa Wilaya Tandahimba
3.	Ndg:	Mohamedi A. Fakili	-Katibu Tawala (W)
4.	“	Thomas Mhecha	-Afisa Usalama (W)
5.	“	Juma A. Lusasi	-Afisa Tarafa Mahuta
6.	“	Rehema Hoza	-Afisa Tarafa Litehu
7.	“	Born Minga	-Afisa Tarafa Namikupa
8.	“	Mbaraka Hittu	-Katibu CUF (W)
9.	“	Abdallah Nalinga	-Mwenyekiti CHADEMA (W)
10.	“	Willy Mkapa	-Katibu CHADEMA (W)
11.	“	Mohamedi Manyamba	-Katibu CCM (W)
12.	“	Ally S. Muwanya	-Mwenyekiti wa Mji Mdogo Tandahimba

D: SEKRETARIATI

1. Christian Mazuge
2. Sofia Nanjota
3. Mohamedi Namkuva

MUHT.NA. 04/2016/2017- KUFUNGUA KIKAO

Wajumbe kabla ya kikao kufunguliwa waliimba wimbo wa Taifa wakiongozwa na Mwenyekiti. Katibu alieleza kuwa akidi imetimia hivyo alimkaribisha mwenyekiti afungue kikao. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kisha alifungua kikao saa 05:28 asubuhi.

MUHT.NA. 05/2016/2017- KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda kumi na nne (14) zilizoandaliwa ziliwasilishwa mbele ya wajumbe wa kikao kwa ajili ya kuzipitia.Baada ya kuzipitia wajumbe waliridhia agenda hizo ambazo ni:-

SIKU YA KWANZA YA BARAZA TAREHE 27/10/2016

1. Kufungua kikao cha Baraza la Madiwani
2. Kuthibitisha Agenda za kikao cha Baraza la Madiwani
3. Kupitia taarifa mbalimbali za miradi ya maendeleo ya Kata

SIKU YA PILI YA BARAZA TAREHE 29/07/2016

4. Kujibu maswali ya Wahe. Madiwani ya papo kwa papo
5. Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 28-29/07/2016 na tarehe 29/09/2016
6. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
7. Kujibu maswali ya Waheshimiwa Madiwani ya Maandishi
8. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya kipindi cha Robo ya kwanza (Julai- Septemba 2016/2017)
9. Taarifa mbalimbali za kamati za kudumu za Halmashauri ya Wilaya
    a) Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi
    b) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    c) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    d) Kamati ya Kudhibiti UKIMWI
10. Maombi ya kuanzisha duka la dawa za binadamu
11. Taarifa ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)
12. Kutoa uwakala wa kukusanya ushuru unaotokana na zao la korosho na fedha za Mfuko wa Elimu
13. Taarifa za Kiutumishi
14. Kufunga kikao

MUHT.NA. 06/2016/2017- KUPITIA TAARIFA MBALIMBALI ZA MIRADI YA MAENDELEO YA KATA

Mwenyekiti alitoa pendekezo la kujadili taarifa za kata chache ili kuleta ufanisi. Wajumbe waliridhia na kisha kata zilizoteuliwa ziliwasilisha taarifa kama ifuatavyo:-

KATA YA MAHUTA

Mh. Diwani alisisitiza juu ya ujenzi wa shule ya Sekondari kata ya Mahuta, umaliziaji wa ofisi ya kata na ujenzi wa nyumba ya Mtendaji Kata.

KATA YA MNYAWA

Iliridhiwa

KATA YA MALOPOKELO
Mjumbe alihoji juu ya ofisi za kata kutengewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Katibu aliahidi bajeti ikivuka makadirio kutoa fedha kwenye kata. Pia alipongeza jitihada za kata hiyo kwa kupunguza tatizo la mimba kwa wanafunzi na kushauri madiwani wote wapambane kupunguza mimba kwa wanafunzi.

KATA YA LUAGALA
Kutokana na tatizo la walimu wa sayansi na hesabu katika kata hiyo, Katibu alishauri uongozi wa kata utafute suluhisho la muda kwa kutafuta walimu wa muda na kuwapa ushirikiano walimu waliopo ili kukabiliana na tatizo hilo.

KATA YA NAMIKUPA
Mh. Diwani wa kata hiyo alieleza kuwa wananchi wameanzisha ujenzi wa shule ya Msingi katika kijiji cha Pemba na kueleza kuwa kumekuwa na changamoto kutoka kwa wanasiasa.

USHAURI
Katibu alishauri wanasiasa wasikwamishe jitihada za wannanchi katika shughuli za maendeleo.

KATA YA MICHENJELE
Mh. Diwani alieleza juu ya tatizo la watoa huduma za Afya katika zahanati ya Michenjele. Katibu alikili juu ya kuwepo kwa taizo hilo na kueleza kuwa bajeti imetengwa hivyo watumishi hao wanasubiriwa hadi watakapoletwa na serikali.

Katibu aliahidi pia kulifanyia kazi tatizo la umeme kwenye jingo la uzazi katika zahanati hiyo ya Michenjele.

ANGALIZO
Mwenyekiti alitoa angalizo na kushauri wananchi waishi vizuri na watoa huduma za Afya kwani kumekuwa na matukio mabaya wanayofanyiwa watoa huduma hao hali inayopunguza ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

Katibu alishauri pia wauguzi (ndugu wa wagonjwa) wasiwe wengi kwenye maeneo ya kutolea huduma ili kurahisisha utendaji kazi wa watoa huduma. Pia alihimiza juu ya uhamasishaji wa wananchi ili wajiunge na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na kueleza kuwa kwa siku za usoni kutakuwa na shindano la kupata kata zitakazokuwa na wanachama wengi wa CHF.

KATA YA MILONGODI
Taarifa ilipokelewa na kuridhiwa.

KATA YA NGUNJA

Mh. Diwani aliomba fedha za wanafunzi hewa zirejeshwe kwani wanafunzi hao wamerejea shuleni. Alieleza pia juu ya wanachama wa CHF kutopata vitambulisho pamoja na tatizo la maji katika kata hiyo. Katibu alieleza kuwa suala la wanafunzi hewa halikuwa na namna ya kuzuia, kuhusu tatizo la maji litafanyiwa kazi na Mhandisi wa Maji (W) na suala la vitambulisho vya CHF alieleza kuwa hadi mwezi Novemba vitakuwa vimekamilika.

Mjumbe alihoji kama wazee zaidi ya miaka sitini wanaweza kujiunga na CHF. Ilielezwa kuwa wazee wa miaka sitini hawahusiki na mpango wa CHF ila wanaweza kujiunga kama wana wategemezi ili wapate huduma.

KATA YA MIUTA

Mjumbe alihoji juu ya wanafunzi kutokaa bwenini katika shule ya Sekondari Kitama. Mh. Diwani wa kata hiyo aliomba madiwani wa kata zingine kuhmasisha wanafunzi kukaa bwenini kwani wanafunzi wa shule hiyo wanatoka katika kata tofauti ndani ya Wilaya.

KATA YA MKUNDI

Mjumbe alihoji juu ya mwenyekiti wa kijiji aliyehukumiwa kifungo kama bado yupo kazini. Mh. Diwani alieleza kuwa mtumishi huyo hayupo kazini tangu alipohukumiiwa kifungo.

Mjumbe mwingine alihoji kama maji ya chanzo cha Chitoholi hayawezi kkutumiwa kwa matumizi ya binadamu. Kaimu Mhandisi wa Maji (W) alieleza kuwa maji hayo yanatakiwa yapimwe kabla la kuruhuru kutumiwa na binadamu.

Katibu alishauri madiwani wasimamie watendaji wa kata ili watumie mapato ya kata zao kuandaa taarifa za kuwasilisha kwenye vikao.

Mwenyekiti alisisitiza madiwani kuandaa taarifa za kata zao na kuziwasilisha kwenye kikao. Kikao kiliahirishwa saa 07:42 mchana kwa siku ya kwanza.

SIKU YA PILI YA BARAZA TAREHE 28/10/2016

MUHT.NA. 07/2016/2017- KUJIBU MASWALI YA WAHE, MADIWANI YA PAPO KWA PAPO

Wajumbe walipewa nafasi ya kuuliza maswali ya papo kwa papo. Maswali yaliyoulizwa ni kama ifuatavyo:-

SWALI

Mh. Diwani wa Tandahimba alihoji Halmashauri ina utaratibu gani wa kupima viwanja eneo la ikulu ndogo na eneo la Matogoro.

JIBU
Katibu alijibu kuwa suala hilo limeanza kufanyiwa kazi kwa kumkaimisha Ofisi Afisa Mipango Miji ili ashughulikie changamoto hizo.

SWALI
Mh. Diwani wa kata ya Malopokelo aliuliza kama kuna mikakati ya kutenga wodi ya wagonjwa wa kutengwa kwani ni hatari kwa wagonjwa wengine.

JIBU
Katibu alieleza kuwa wataalam watatafuta ufumbuzi kwa kufanya tathmini ya athari na ikionekana kuna athari eneo jipya litaombwa kwa ajili ya kujenga wodi ya wagonjwa wa kutengwa.

MUHT.NA. 08/2016/2017- KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 28-29/07/2016 NA TAREHE 29/09/2016
Mihtasari ya vikao vya Baraza la madiwani vya tarehe 28-29/07/2016 na tarehe 29/09/2016 iliwasilishwa kwa ajili ya kuipitia na kuithibitisha. Mara baada ya wajumbe kuipitia mihtasari hiyo, walikubali kuwa vilivyoandikwa ni kumbukumbu sahihi za vikao hivyo.

MUHT.NA. 09/2016/2017- TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)
Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa yake mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa hiyo ilieleza mambo yafuatayo:-

1. **USAJILI NA UHAKIKI WA VITAMBULISHO VYA TAIFA KWA WATUMISHI WA UMMA**
   Alieleza kuwa zoezi hilo lilianza tarehe 03/10/2016 ambapo watumishi 1697 walikuwa wameshasajiliwa, watumishi 428 vitambulisho vyao vimehakikiwa na wengine 160 walikuwa bado wanahakikiwa ili kupata jumla ya watumishi 2285.

2. **UHAKIKI WA VYETI KWA WATUMISHI WA UMMA**
   Katika kutekeleza agizo la serikali juu ya uhakiki wav yeti vya Sekondari na taaluma kwa watumishi wa umma, Halmashauri imetekeleza agizo hilo na kuwasilisha nakala lainina nakala ngumu za vyeti vya watumishi kwa Baraza la Mitihani la Taifa tarehe 13/10/2016. Baada ya Baraza la mitihani kuwasilisha ripoti ya matokeo ya uhakiki huo kwa Mkurugenzi Mtendaji (W), ripoti hiyo itawasilishwa katika vikao vya baraza la madiwani.

3. **TAARIFA YA MAANDALIZI YA MSIMU WA UNUNUZI NA UUZAJI WA KOROSHO GHAFI 2016/2017.**
   Msimu wa mauzo ya korosho ulifunguliwa rasmi tarehe 01/09/2016 na hadi tarehe ya kikao kilo 38,024 zilikusanywa na kuuzwa kwa bei ya shilingi 3,670. Hadi tarehe

18/10/2016 minada miwili Changamoto iliyojitokeza ni korosho kupelekwa kuuzwa zikiwa na unyevu hali iliyopunguza ubora wa korosho hizo.

4. UJIO WA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN

Mnamo tarehe 09/09/2016 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilimpokea Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kukagua na kujionea utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Wilaya ya Tandahimba. Akiwa Tandahimba Mhe. Samia Suluhu Hassan aliweza kukagua shughuli za uendeshaji wa kiwanda cha kubangua korosho cha AMAMA FARM katika kuongeza thamani katika zao la korosho. Pia alipata fursa ya kutoa zawadi kwa shule ya Sekondari Tandahimba ilishika nafasi ya 10 katika matokeo ya mitihani ya kidato cha sita mwaka 2016.

5. UJIO WA WAZIRI WA ELIMU PROF. JOYCE NDALICHAKO

Waziri wa Elimu Sayansi na Teknologia Prof. Joyce Ndalichako alifika Tandahimba na kuipongeza Shule ya Sekondari Tandahimba kwa matokeo mazuri ya mitihani ya kidato cha sita na kuahidi kujenga nyumba 5 za walimu fedha ambazo zitatoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Aidha Mh. Waziri alipata fursa ya kutembelea mradi wa nyumba moja yenye kuishi walimu sita katika shule ya Sekondari Michenjele na kupongeza viwango vya ujenzi na kusisitiza kukamilisha mradi kwa wakati.

Kuhusu wanafunzi hewa, matokeo ya uhakiki yalionesha kuwa wanafunzi waliosajiriwa mwezi machi, 31 2016 walikuwa 7428, waliokuwepo shuleni 7328 na kupata tofauti ya wanafunzi 100 ambao walikuwa na sababu mbalimbali zikiwemo kuhama, utoro na kufariki.

6. UENDESHAJI WA MITIHANI YA DARASA LA SABA

Mitihani ya kumaliza elimu ya msingi mwaka 2016 ilifanyika tarehe 7-9/09/2016 kama ilivyokuwa imepangwa na Baraza la Mitihani la Taifa. Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilikuwa na jumla ya shule 118 kati ya shule 125 zilizokuwa na watahiniwa wa mitihani hiyo. Jumla ya watahiniwa 4874 walisajiriwa kufanya mitihani kati yao wasichana 2702 na wavulana 2172. Watahiniwa waliofanya mitihani ni 4849 kati yao wavulana 2159 na wasichana ni 2690 sawa na asilimia 99.5.

Taarifa ilipkelewa

MUHT.NA. 10/2016/2017- KUJIBU MASWALI YA WAHE. MADIWANI YA MAANDISHI

Maswali ya maandishi hayakuwasilishwa.

MUHT.NA. 11/2016/2017- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI- SEPTEMBA 2016/2017)

Afisa Mipango alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imeidhinishiwa kupokea na kutumia jumla ya shilingi 8,356,065,970.00/= katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia , Dira ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2025 (vision 2015), Sera mbalimbali za kisekta pamoja na malengo ya maendeleo endelevu (SDG's). Hii ni kutokana na dira na dhima ya Halmashauri kwamba***"Ifikapo 2018 halmashauri ya wilaya ya Tandahimba , kwa kutumia rasilimali zilizopo, utaalam na ushirikishaji wa jamii, iwe imetoa huduma bora kujenga uchumi endelevu utakaowezesha maisha bora ya wananchi"***

Fedha hizo zilitarajiwa kuchangiwa na wadau mbalimbali ikiwemo mapato ya ndani ya Halmashauri (Ownsource), ruzuku ya maendeleo toka serikali kuu (LGCDG), mfuko wa barabara (Road Fund), mfuko kabambe wa afya (health Sector Basket Fund), mfuko wa maji (RWSSP), mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari (Word Bank), Mpango wa maendeleo Elimu Msingi(PEDP), EGPAF, Mfuko wa Jimbo, Pamoja na mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF).

Mchanganuo wa fedha hizo kwa wachangiaji hapo juu kwa mwaka 2015/2016 ni kama unavyoonekana kwenye jedwali hili:-

NA	**CHANZO/MCHANGIAJI**	MAKISIO	**FEDHA TOLEWA**	**FEDHA TUMIKA**	**FEDHA ZISIZOPOKELEWA**	**% YA FEDHA POKELEWA**
1	OWNSOURCE	3,304,250,000.00			3,304,250,000.00	
2	LGCDG	818,851,000.00			818,851,000.00	
3	MFUKO WA MAJI (NRWSSP)	299,440,000.00			299,440,000.00	
4	ROAD FUND	1,222,290,000.00			1,222,290,000.00	
5	BASKET FUND	484,556.000.00			484,556.000.00	
6	PEDP	100,000,000.00			100,000,000.00	
7	MFUKO WA JIMBO	46,991,000.00			46,991,000.00	
8	TASAF	1,459,485,000.00	461,830,500.00	407,636,000.00	1,229,116,500.00	15%
9	WORD BANK	578,164,000.00			578,164,000.00	
10	EGPAF	42,038,970.00	42,038,970.00		42,038,970.00	100%
	JUMLA	**8,356,065,970.00**	**503,869,470.00**	407,636,000.00	**7,852,196,500.00**	**6.03%**

Hadi kufikia tarehe 30/09/2016, Halmashauri ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi **503,869,470.00** katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 6.03 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017

Aidha kupitia mfuko wa maendeleo ya jamii TASAF katika robo ya kwanza Halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. 461,830,500.00 na kutumia jumla Tshs. 407,636,000.00 kwa ajili ya malipo ya kaya masikini. Hata hivyo Tshs. 2,880,000.00 zimerejeshwa TASAF Makao Makuu kutokana baadhi ya walengwa kukosa sifa za kulipwa fedha hizo kutokana na vifo au kuhama makazi.

Hadi kufikia tarehe 30/09/2016 Halmashauri imepokea shilingi 199,454,491.30 toka mfuko wa barabara kwa ajili ya utekelezaji wa mairadi ya barabara kwa mwaka 2015/2016.

Taarifa ilipokelewa.

YALIYOJITOKEZA

Mjumbe aliomba ufafanuzi juu ya kamati inayohusika kutembelea miradi. Mwenyekiti alifafanua kwa kusema kuwa Kamati ya fedha, Mipango na Uongozi ndiyo inayohusika kutembelea miradi kwa mujibu wa mwongozo na wenyeviti wa Kamati walipewa taarifa.

Mjumbe alihoji juu ya mradi wa kutengeneza madawati kwani madawati tayari yametosha. Afisa Mipango (W) alieleza kuwa bajeti ilipangwa kabla ya madawati kutosha na pia wanafunzi wamekuwa wakiongezeka na kueleza kuwa kama hakutakuwa na haja ya madawati fedha hizo zitabadirishiwa matumizi.

USHAURI

Kikao kilishauri kwa miradi ambayo haijapata fedha kutoka Serikali kuu, itekelezwe fedha zitakapofika na pia wahusika wakumbushwe ili fedha zifike.

Mjumbe aliongeza kwa kusema kuwa hata miradi ya mapato ya ndani haijaanza kutekelezwa hadi hapo fedha zitakapokusanywa.

MUHT.NA. 12/2016/2017- TAARIFA MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA

I. KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI

Mwenyekiti wa kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi aliwasilisha taarifa hiyo mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa ilieleza jinsi kamati ya fedha ilivyofanya vikao na agenda zilizojadiliwa. Pamoja na taarifa, iliambatanishwa mihtasari ya vikao vya kamati hiyo na taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Septemba, 2016.
Taarifa ilipokelewa.

YALIYOJITOKEZA

Mjumbe alihoji juu ya watumishi wa Halmashauri kupewa zabuni za kuchapisha na kudurufu nyaraka za ofisi. Ilielezwa kuwa Bodi ya Zabuni haikugundua kuwa wazabuni hao ni watumishi . Katibu aliahidi kuwaondoa ikithibitika kuwa ni watumishi wa Halmashauri.

Mjumbe alihoji juu ya mapato ya Mfuko wa Elimu shilingi 10,000,000/= kutoonekana kwenye matumizi. Mweka Hazina (W) alieleza kuwa fedha hizo hazikutumika.

Mjumbe alihoji juu ya manunuzi ya dawa nje ya Bohari ya Dawa (MSD). Afisa Manunuzi alieleza kuwa dawa ambazo zilikosekana kwenye Bohari ya Dawa ndizo zilizonunuliwa nje kwa kufuata taratibu husika.

KUHUSU MKATABA WA KUKODISHA JENGO KWA TACOBA

Katibu alieleza kuwa mazungumzo kati ya Benki ya TACOBA na Halmashauri yanaendelea hivyo yatakapokamilika taarifa itawasiliswa kwenye vikao.

II. KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI

Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji aliwasilisha taarifa ya kamati hiyo mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa ilieleza jinsi kamati ya Elimu, Afya na Maji ilivyofanya vikao vyake. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo cha tarehe 19/07/2016.

III. KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa iliyoeleza jinsi vikao vya kamati hiyo vilivyofanyika. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo cha tarehe 18/07/2016.
Taarifa ilipokelewa.

YALIYOJITOKEZA

Wajumbe walieleza kuwa maandalizi ya nane nane 2016 hayakuwa mazuri kwa upande wa usafiri na posho za madiwani pamoja na kuwa na utambulisho na kushauri maboresho yafanyike kwa miaka ijayo.

Katibu alieleza kuwa sherehe hiyo haikuwepo kwenye bajeti hivyo maboresho yatakuwepo kwa miaka ijayo.

Mjumbe alieleza kuwa viongozi wa vyama vya msingi wengi wao si waadilifu na kushauri wananchi wasikilizwe wanapotoa malalamiko yao.

SUALA LA VITAMBULISHO VYA MADIWANI

Katibu aliahidi kuviandaa na kuwapatia madiwani kabla ya Baraza la madiwani mwezi Januari, 2016.

IV. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa kamati ya Kudhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa hiyo mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa ilieleza jinsi kamati hiyo ilivyofanya vikao vyake. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo wa tarehe 15/07/2016.
Taarifa ilipokelewa.

MUHT.NA. 13/2016/2017- MAOMBI YA KUANZISHA DUKA LA DAWA ZA BINADAMU

Mganga Mkuu (W) aliwasilisha taarifa fupi ya kuanzisha duka la dawa za binadamu na Umuhimu wake. Uanzishaji wa duka hili utategemea Mkopo kutoka Bima ya Afya ya Taifa na Mchango wa Halmashauri, pia Halmashauri itafanya ukarabati wa jengo litakalotumika kama duka la Dawa za Binadamu kwa muda.
Taarifa ilipokelewa na kuridhiwa.

YALIYOJITOKEZA

Wajumbe waliunga mkono hoja na kushauri dawa ambazo hazitolewi na Bima ya Afya nazo ziwepo.

TAARIFA

Mjumbe alihoji juu ya uendeshaji wa duka la dawa litakaloanzishwa. Katibu alieleza kuwa kutakuwa na chombo maalum kitakachoundwa kwa ushirikiano na Kamati Elimu, Afya na Maji.

MUHT.NA. 14/2016/2017- TAARIFA YA MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

Ifuatayo ni mikakati itakayowezesha Halmashauri kuongeza idado ya wananchi kujiunga na mfuko wa bima ya afya ya jamii (CHF).

1. Kuwepo kwa dawa za kutosha na vifaa tiba katika vituo vyote vya kutolea huduma kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya Afya na hospitali ya Wilaya.
2. Kushirikisha viongozi katika ngazi zote akiwemo mkuu wa Wilaya, Mbunge, Madiwani, Watendaji wotewa ugani ili kuweka azimio la pamoja na kuhakikisha kila kaya katika kijiji husika wanajiunga na mfuko wa Bima ya Afya ya jamii.
3. Halmashauri kupitia makusanyo yake ya ndani itoe fungu la fedha ili kuweza kufanya uhamasishaji katika vijiji vyote ili kujenga uelewa miongoni mwa jamii juu ya umuhimu wa kujiunga na mfuko.
4. Kuhamasisha Kaya Makundi ili kujiunga na mfuko huu.
5. Halmashauri iwalipie wazee CHF ili wapate kadi za matibabu.
6. Kuimarisha zaidi mfumo wa ukusanyaji fedha za CHF.
7. Kitengo cha TASAF kiridhie kuwalipia wanufaika wote wa Kaya Maskini wanaopewa ruzuku ili wajiunge na CHF.

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.

MUHT.NA. 15/2016/2017- KUTOA UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU UNAOTOKANA NA ZAO LA KOROSHO NA FEDHA ZA MFUKO WA ELIMU

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha mapendekezo ya kutoa uwakala wa kukusanya ushuru unaotokana na zao la korosho na fedha za Mfuko Wa Elimu kwa chama kikuu cha Ushirika Newala na Tandahimba (TANECU). Alieleza kuwa kwa muda mrefu Halmashauri imekuwa na mgogoro na vyama vya msingi juu ya ulipaji wa ushuru wa zao la korosho.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2016,Halmashauri ilikuwa inavidai vyama vya msingi shilingi 1, 859,217,958.96 kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009 hadi 2015/2016. Ilielezwa kuwa hali hiyo imekuwa ikikwamisha utendaji wa Halmashauri katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Ili kuepuka tatizo la kutokusanya ushuru wa zao la korosho kwa ukamilifu pamoja na kupunguza migogoro kati ya Halmashauri na vyama vya msingi, menejimenti ilipendekeza kutoa uwakala kwa TANECU ambao ndio wasimamizi wa vyama vya msingi. Malipo ya mkataba yanatarajiwa kuwa 1% ya kiasi ambacho wakala atakusanya na kusasilisha Halmashauri.
Taarifa ilipokelewa

YALIYOJITOKEZA
Mwenyekiti alifafanua kuwa kwa kuwa TANECU ndiyo walezi wa vyama vya Msingi itasaidia kupata mapato ya ushuru kutoka kwenye vyama hivyo vya Msingi na pia msisitizo utawekwa ili wakishindwa kukusanya Halmashauri ikusanye yenyewe.Mjumbe alishauri TANECU ipewe na jukumu la kukusanya madeni ya nyuma ya vyama vya Msingi.

HITIMISHO
Kikao kilihitimisha na kukubaliana kuwa madeni ya nyuma yafuatiliwe na Afisa Ushirika na Mweka Hazina (W)

USHAURI
Kikao kilishauri mkataba uharakishwe na pia muda wa kuvunja mkataba uwe mfupi ili Halmashauri isiporidhika na ukusanyaji ikusanye yenyewe.

SUALA LA USHURU WA VIJIJI
Mjumbe alihoji juu ya makato ya ushuru wa vijiji kutoka kwenye zao la korosho. Ilielezwa kuwa viongozi wa kata na vijiji ndio wahusika wa kusimamia makato hayo kwa makubaliano na wananchi.

MUHT.NA. 16/2016/2017- TAARIFA ZA KIUTUMISHI
Taarifa haikuwasilishwa

NASAHA ZA MKUU WA WILAYA
Mkuu wa Wilaya aliwapongeza wajumbe kwa kujadili mambo ya maendeleo na kuhimiza juu ya elimu ili wananchi wawe na uelewa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

SUALA LA VYAMA VYA MSINGI
Alieleza kuwa vyama vya Msingi vina changamoto nyingi ikiwemo ubadhilifu na kueleza kuwa sheria inataka kila chama kifanye kazi kwenye eneo lake. Aliongeza kwa kusema

kuwa vyama hivyo vinaongozwa na sheria hivyo wabadhilifu watawajibishwa kwa mujibu wa sheria. Aliwasihi madiwani kutobadili uongozi wa vyama vya msingi ili wasiharibu utaratibu kwa haraka katikati ya msimu wa mauzo ya korosho.

KUKABILIANA NA NJAA
Aliwasihi madiwani wahamasishe wananchi walime mazao ya chakula angalau kila kaya iwe na hekta mbili za mazao ya chakula kamavile muhogo, mtama na mahindi.

Alihimiza pia juu ya utunzaji wa korosho kabla ya kupeleka ghalani na kuhimiza maafisa Ushirika kusimamia ili korosho zifikishwe maghalani zikiwa na ubora na kukwepa udanganyifu kwenye mizani.

FEDHA ZA PEMBEJEO
Mkuu wa Wilaya aliagiza Afisa Ushirika awasilishe taarifa ya fedha za pembejeo na matumizi yake.

SUALA LA WANANCHI KUHAMIA MSUMBIJI
Mkuu wa Wilaya aliwasihi wananchi wasikimbilie Msumbiji bila kuwa na Shughuli maalum.

KUHUSU JANGA LA UKIMWI
Aliwasihi wananchi kujiepusha na tabia hatarishi zinazosababisha maambukizi ya UKIMWI ili kulinda nguvu kazi.

MUHT.NA. 17/2016/2017- KUFUNGA KIKAO
Katibu alieleza kuwa agenda zilizoandaliwa zimeshajadiliwa hivyo alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti aliwasihi madiwani kufikisha yaliyojadiliwa kwa wananchi. Aliomba Mkuu wa Wilaya awashirikishe madiwani kwa masuala yanayotokea ndani ya kata zao ili kuleta ufanisi. Alihimiza uharakishwaji wa malipo ya fedha za wakulima waliouza korosho zao ili kudhibiti kangomba.Kikao kilifungwa saa 06:58 mchana.